

Kundi la pili ni samaki ambao hawapendelei kuishi kwenye mawe na ambao pia wengi wao hutumika kwa kitoweo na wako chini ya koo (genera) 38. Hata hivyo wizara ya mifugo na uvuvi inaendelea na utafiti kubaini wingi na idadi ya samaki wa mapambo katika Ziwa Nyasa kupitia Taasisi yake ya utafiti (TAFIRI).

5. MAENEO YA MADINI

Wilaya ya Nyasa inayo hazina y madini ya dhahabu yanayopatikana katika maeneo ya Kijiji cha Lunyele, Tarafa ya Mpepo



6. MAENEO YA UTALI (BANDARI, MAENEO YA FUKWE REC-REATIONAL SITES NA MAPANGO)

Mwambao wa Ziwa Nyasa ni moja ya vivutio kwa watalii wa ndani ya nchi na nje ya nchi ya Tanzania kutokana na uwepo wa fukwe na visiwa ndani ya ziwa,



7. JIWE LA POMONDA LA LIULI



Hili jiwe lilitumika wakati wa vita likitumika kwa ajili ya kujificha dhidi ya adui, kuna mapango ambayo yalitumika kwa kujificha.

8. VYANZO VYA MAJI VYA KUTOSHA



Kwa Mawasiliano

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya
Halmashauri ya Wilaya
S.L.P. 90
Nyasa

Simu : 0252673005
Nukushi : 0252673005
Barua pepe : dednyasa2014@gmail.com

**JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA
MITAA**

**MKOA WA RUVUMA
HALMASHAURI YA WILAYA YA
NYASA**



**VIVUTIO VYA UWE-
KEZAJI WILAYA YA NY-
ASA**



HALMASHAURI YA NYASA VIVUTIO VYA WILAYA

USULI WA WILAYA

Wilaya ya Nyasa yenye ukubwa wa kilomita za Mraba 6790. Ilianzishwa tarehe 8/03/2012 kwa tangazo la Gazeti la Serikali Na. 87, Aidha Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa imeanzishwa baada ya kuigawa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa ni moja kati ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Ruvuma. Sheria Na. 7 ya mwaka 1982 iliwezesha kuanzishwa kwa Halmashauri hii tarehe 01/07/2013.

Wilaya ya Nyasa ipo kati ya latitudo 10° 15" na 11° 34" kusini mwa mstari wa ikweta na longitudo 34° 24" na 35° 28" mashariki. Wilaya inapakana na Wilaya ya Mbinga kwa upande wa Mashariki, Jamhuri ya Msumbiji upande wa Kusini, Ziwa Nyasa upande wa Magharibi na Wilaya ya Ludewa upande wa Kaskazini.

Kwa mujibu wa sensa ya Mwaka 2012 inakadiriwa Wilaya kuwa na idadi ya watu 146,160, wanaume ni 71,392 na wanawake ni 74,768.

Wilaya ina tarafa 3, kata 20, vijiji 84 na vitongoji 425. Hali ya hewa ni ya baridi isipokuwa maeneo ya mwambao wa ziwa Nyasa ambapo ni ya joto karibu majira yote ya mwaka. Kiwango cha juu cha joto inakadiriwa kuwa kati ya 29°C na 31°C na kiwango cha chini ni 19°C na 23°C. Kipindi cha baridi kinaanza mwezi June hadi Agasti.

Wilaya ya Nyasa ina miinuko kwa upande unaolekea Matengo wastani wa mwinuko wa meta 2000 na tamabarare kwa maeneo ya mwambao wa Nyasa kati ya meta 900 na meta 1300 toka usawa wa bahari.

DHIMA NA DHAMIRA YA WILAYA

DHIMA YA WILAYA

Kuwa Halmashauri kiongozi kwenye utoaji wa huduma bora na uboreshaji wa shughuli za kiuchumi kwa jamii

DHAMIRA YA WILAYA

Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa imedhamiria kuongoza na kuwezesha jamii kwenye Maendeleo Katika Nyanja za Kiuchumi, Kijamii, Kiutamaduni na Kimazingira kwa njia endelevu na ushirikishwaji Mkubwa.

VIVUTIO VYA WILAYA

Wilaya ya Nyasa ina hazina ya vivutio vyenye tija kwa maendeleo ya kiuchumi.

1. MILIMA (LIVINGSTONE RANGE—SAFU ZA KIPENGELE) NA MBUGA ZA WANAYAMA

Milima ya Livingstone yenye mwinuko wa kufikia meta kutoka usawa wa bahari 2000, milima hii inatambaa kutoka upande wa Kusini mwa Wilaya kuelekea kaskazini.



2. ARDHI YENYE RUTUBA KWA KILIMO

UKANDA WA MILIMA YA MATENGO

Tarafa ya Mpepo ina utajiri mkubwa wa kilimo hususani mazao ya mahindi, maharagwe, soya, ngano, mtama, tumbaku na kahawa. Zao kuu la biashara ni zao la Kahawa linalolimwa katika maeneo ya Kata za **Luhangarasi, Tingi, Kingerikiti** na **Liparamba**.



Eneo linalofaa kwa kilimo cha nafaka ni Km za mraba 78,162

Eneo linalofaa kwa Kilimo cha Kahawa ni Km za mraba 31,680



UKANDA WA MWAMBAO WA NYASA

Eneo hili liko kati ya Bonde la Hagati na Ziwa Nyasa lenye wingi wa rutuba itokanayo na uoto wa asili wa miti ya miombo na nyasi. Eneo hili ni kubwa na ni bora kwa kilimo cha **mpunga, mahindi, muhogo**, Korosho, **ndizi** na **miwa na uvuvi**. Muhogo ni zao kubwa la chakula katika ukanda huu

3. ZIWA NYASA

Ziwa Nyasa ni ziwa la tatu kwa ukubwa na la pili kwa kina katika Afrika, Pia ni Ziwa la tisa kwa ukubwa Ulimwenguni Ziwa hilo lipo kwenye usawa wa meta 500 toka usawa wa bahari ambapo kina cha ziwa hilo ni karibu meta 750, urefu wake ni karibu kilometa 1000. limezungukwa na nchi tatu ambazo ni Tanzania, Malawi na Msumbiji.

4. UVUVI WA SAMAKI

Ziwa hili ndilo lenye aina nyingi za samaki kuliko aina zote za maji baridi ikiwa na aina tofauti za samaki



5. SAMAKI WENYE MAPAMBO—LIULI

Taarifa ya wizara ya uvuvi na Maendeleo ya Mifugo nchini inaonyesha kuwa samaki wanaovuliwa kwa ajili ya biashara ya samaki wa mapambo kutoka Ziwa Nyasa wamegawanyika katika makundi mawili makubwa ambayo ni samaki wale wanaoishi zaidi kwenye mawe au miamba ambao kuna aina (species) zipatazo 250.